## EPISODE 3 "SURFING AND SCRATCHING"

**SCRIPT WRITER** **Njoki Muhoho**

**EDITOR** **Jan-Philipp Scholz**

**KISUAHELI** **Eric Ponda**

**CHARACTERS**

| | |
|---|---|
| **ANNOUNCER** | Male Adult |
| **ZAPCOM** | A 23-year-old computer geek, by village standards. |
| **GEORGE** | 20 years old. Waits tables at his Uncle Kilu's restaurant. |
| **MUMBI** | 22 years old, Zapcom's cousin and social worker. Female. |
| **ISP TECHY** | 28 year old ISP technician |
| **UNCLE KILU** | 55 years old. George's uncle, owner of KULA TU FOODS. |
| **OMWA** | 19 years old and jobless. Female. |
| **YOUNG MAN** | 19-year-old internet enthusiast |

**INTRO**

**1.** MUSIC: THEME MUSIC

***2.*** ANNOUNCER HUJAMBO MSIKILIZAJI NA KWA MARA NYINGINE KARIBU KWA MAKALA NYINGINE YA MCHEZO WA REDIO "LEARNING BY EAR", 'NOA BONGO JENGA MAISHA YAKO',

KUHUSU TEKNOLOJIA MPYA YA HABARI NA MAWASILIANO KWA JINA ‘UTAFITI WA MTANDAO YAANI ***SURFING AND SCRATCHING.’***

KATIKA KIPINDI KILICHOTANGULIA, ZAPCOM ANAPATA KOMPUTA YA KWANZA KUANZISHA MRADI WAKE WA HUDUMA ZA INTANETI. BA-MDOGO KILU ANANZA KUHOJI BAADA YA KUFAHAMU KWAMBA PIA ANAWEZA KUIMARISHA BIASHARA YAKE KUPITIA HUDUMA HIZI ZA MTANDAO WA INTANETI.YEYE PAMOJA NA KUNDI HILO VIJANA WAFIKIANA KUANZISHA USHIRIKA WA KIBIASHARA. JE USHIRIKIANO HUU WA WAZEE NA VIJANA UTAFAULU KUPAMBANA NA CHANGAMOTO ZINAZOANDAMANA NA BIASHARA YENYEWE? ENDELA KUWA NASI USIKIE YATAKAYOJIRI.

**SCENE 1: KULA TU FOODS**

**3. A-SFX: NORMAL MURMURING IN A RESTAURANT ON A SLOW DAY.**

**4. UNCLE KILU** (**LOUD WHISPHER**) Hebu niambie, wateja wote hawa wametoka wapi?

**5. ZAPCOM** **(DISTRACTED)** ISP

**6.** **UNCLE KILU** Maana ya Iespee ni nini?

**7.** **GEORGE** Ina maana mtoaji wa huduma za mtandao wa Intaneti yaani ***internet Service Provider***.Ni kampuni inayotoa huduma za Intaneti kwa wateja wake. Hutumia teknolojia ya masafa marefu kupeperusha mawasiliano hivyo kuwawezesha wateja kubadilishana habari na kuwasiliana na ulimwengu mzima kwa urahisi.

**8.** **UNCLE KILU** (**DAZZLED AND AMUSED**). Allalllalala, sasa Ulimwengu mzima umenishukia,…. mimi Kilu, niko na ulimwengu mzima hapa tu katika mgahawa huu wangu!.

**9.** **ISP TECHY** (**BIG SIGH OF RELIEF**) Sawa tumekamilisha. Uko tayari sasa? (**COMPUTER KEY BOARD TAPPING**). Wewe pamoja na wateja wako sasa mumeweza kuunganishwa na ulimwengu mzima. Munaweza kubadilishana habari au kuwasiliana na yoyote kote ulimwenguni kupitia nyaraka za elektroniki..yaani E-mails, picha za video au hata muziki kupitia mtandao huu!

**10. ZAPCOM** Je wateja wetu wanaweza kutumia mtandao wa G-mail, yahoo na Hotmail?...kupitia mtandao huu.

**11. ANNOUNCER** Misamiati au lugha ya kisayansi inayotumika katika teknolojia hii mpya ya habari na mawasiliano sasa imeanza kuzoeleka na kuwa lugha ya kawaida miongoni mwa kundi hili. Mtaalam anafanya kila juhudi kuwaelimisha wenzake jinsi ya kuunganishwa na kutumia mtandao. Wanashangazwa na kiwango cha habari zinazopatikana kwenye mtandao wa Intaneti. Na mjomba Kilu pia amebaki kinywa wazi!.

**12. ISP TECHY** Ah, Mzee (**REFERING TO UNCLE KILU**) Ungependa kuzuru nchi gani?

**13. UNCLE KILU** (**EXCITED**) Afrika Kusini nchini alikozaliwa shujaa Mandela. (**WITH IRONY**) Kwa nini?

**14. ISP TECHY** George, unaonaje kumtembeza mjombako nchini Africa Kusini sasa hivi hapa. Nenda kwa ***Google***, au ***Yahoo***, utafute ukurasa wowote na uandike "Afrika Kusini" (**QUICK TAPPING OF KEYS**)

**15.** **GEORGE** (**TYPING CONTINUES**) Mjomba nimetamani sana kukupeleka matembezi. Waonaje leo… …hebu tazama kuna kurasa nyingi sana …! zaidi ya 20,000!.

**16.** **ZAPCOM** Neno Afrika Kusini linapatikana katika kurasa nyingi sana. Unaweza kuchagua tu ukurasa wowote miomgoni mwa hizi za kwanza.

**17.** **UNCLE KILU** Sasa tunapiga kambi hapa?

**18.** **ZABCOM** Mtandao si mahali pa kupiga kambi! Ni kama kufungua kitabu kizima cha elektroniki. Ukiwa na mtandao, kwanza unasema nini unachotaka kutafiti, kisha mtandao utatakupa anuani na sehemu zote unazoweza kupata kile unachotafuta. Ndio maana neno Afrika Kusini linapatikana katika kila ukurasa.

**19.** **GEORGE** Mjomba! Kuna njia nyingi zinazoelekea nchini Africa Kusini. Twende tukakutane na Mandela.

**20.** **B-SFX: CHAIR PULLED LOUDLY. HEAVY BODY SITS AND SIGHS. PALMS RUBBING.**

**21.** **UNCLE KILU** Twende!

**22. ANNOUNCER**. MSISISMKO MKUBWA UNALIKUMBA KUNDI ZIMA LA VIJANA KATIKA MKAHAWA WA KULA TU FOODS HUKU LINAPOENDELEA KUJIONEA MAAJABU YA KUTEMBELEA TOVUTI MBALI MBALI ZILIZOMO KWENYE MTANDAO. KUMBUKA HIKI NI KIJIJI CHA MASHAMBANI AMBACHO NDIO MWANZO KIMEANZA SAFARI YA KUTALII NA KUTAFITI MTANDAO WA INTANETI. MUDA SI MUDA WANAFAHAMU KWAMBA MTANDAO WA INTANETI SI MAHALA PA BURUDANI TU, BALI CHANZO CHA HABARI NA MSINGI WA ELIMU.

**SCENE TWO: KULA FOODS RESTRAURANT, END OF WORKDAY**

**23. C-SFX: LOUD NOISES OF PEOPLE EATING AND TYPING OF KEYBOARDS.**

**24. MUMBI** **(IMPATIENT**) Fanya haraka, Omwa!.

**25. OMWA** Si kosa langu, siwezi kupiga chapa kwa haraka! Mimi sikuwa na fedha za kugharamia mafunzo ya kupiga chapa shuleni.

**26. MUMBI** (**ANGRY**) Hiyo ni shida yako, kila wakati wewe hukosi sababu. Endelea kutafuta… andika programu yoyote kwenye Intaneti, sasa anza kufanya mazoezi….! Endapo kila mmoja angeandika kama wewe, biashara yetu ingeporomoka katika muda wa wiki mbili tu.

**27. OMWA** (**EXCITED**) Kwani siwezi kujiunga na chuo cha mafunzo ya kupiga chapa katika mtandao huu?

**28. MUMBI** (**LOSING PATIENCE**) Sasa utajuaje kama huna hata ari ya kutafuta mtandaoni…? Fanya haraka! nataka kutafuta ufadhili kwa miradi ya makundi yangu ya kinamama.

**29. OMWA** (**AMAZED**) Unaweza kupata ufadhili kupitia mtandao pia?

**30. MUMBI** (**EXASPERATED**) Bado una safari ndefu. Una mengi ya kujifunza! Hebu ondoka kwenye komputa.. pia nataka kutumia!

**31. ZAPCOM** Nyinyi wawili fanyeni haraka nataka kutafuta kozi mpya katika shule yangu niliyosomea jijini. Mumemaliza?

**32. D-SFX: APPROACHING QUICK FOOTSTEPS. PANTING.**

**33. YOUNG MAN** (**OUT OF BREATH**). Ha… Sasa kwa hakika tumepata huduma za mtandao wa Intaneti hapa. Fanya haraka pia nataka kujua matokeo ya kandanda barani Ulaya.….Kuna mchuano muhimu ambao umemalizika hivi punde tu…Itanigharimu kiasi gani?

**34. ANNOUNCER** Ingawa ndio mwanzo wa biashara hii, tayari imeshika kasi na kukolea miongoni mwa wanakijiji na wanachohitajika sasa ni kutafuta njia za kuipanua biashara hiyo.

**MUSIC: BRIDGE MUSIC**

**35. UNCLE KILU** (**UNUSUALLY CALM**) Zapu…. Kijana …! unafanya nini lakini? Umezubaa na kushika tama kama mtu mwenye matatizo ya wazee wa rika langu.

**36. ZAPCOM** Nashangazwa na huduma hizi za Intaneti!. Ni za pole pole na bado wateja ni wengi na wanaendelea kumiminika kutafuta huduma hizi. Sijui nifanyeje?

**37. UNCLE KILU** (**SOUNDING WISE**) Najua unachohitaji sasa. **(PAUSE**), Supu ya mbuzi! Wacha nikuletee angalau uchangamke akili!

**38. SFX: FOOT STEPS**

**39. E-SFX: MOBILE PHONE RINGS**

**40. ZAPCOM** Habari kaka Mumbi?. Natumai siku yako ni njema kama yangu!

**41. MUMBI (VO)** (**ON PHONE**) Je kuna komputa ambayo haitumiki kwa sasa, nataka kutumia?

**42. ZAPCOM** (**FLASTERED**) Hata usiulize!

**43. MUMBI (VO)** Ndio sababu nikaamua kupiga simu kwanza kuulizia kabla ya kuja hapo, ili nisifadhaike..

**44. ZAPCOM** **(EXCITED)** Umefanya vyema !... Asante sana .

**45. MUMBI (VO)** (**SURPRISED)** Kwani nini Zapcom?

**46. F-SFX: PANTING, HOBBLING AND CLATTER OF CROCKERY**

**47. ZAPCOM** **(EXCITED**) Kwa kutumia simu yako ya mkononi!

**48. UNCLE KILU** Tayari umeshikwa na msisimko?

**49. ZAPCOM** (**EXCITED, ADDRESSING UNCLE KILU**) Sasa najua nitafanya nini…. (**TO MUMBI**) Wewe njoo tu, njoo haraka, na usisahau kubeba simu yako ya mkononi.

**50. UNCLE KILU** (**SULKY**) Sidhani utakunywa hii supu ya mbuzi saa hii.

**51. ZAPCOM** Hapana wacha hii supu hapa!

**52. ANNOUNCER** ZAPCOM SASA ANAFAHAMU KWAMBA TEKNOLOJIA MPYA YA MAWASILIANO NI CHANGAMOTO NA INAHITAJI MTU KUJITOLEA KWA DHATI.WAZO LAKE SASA LIMESHIKA KASI NA KUWAVUTIA WATU WENGI ZAIDI KIJIJINI. KIMSINGI TEKNOLOJIA HII MPYA NI FURAHA KUBWA KWA YOYOTE YULE MWENYE HIMA YA KUENDELEZA ELIMU YAKE, LICHA YA CHANGAMOTO ZAKE.

**MUSIC: BRIDGE MUSIC**

**SCENE THREE: KULA TU FOODS**

**53. G-SFX: CASH BOX OPENS AND CLOSES. HUM OF BUSY BUSINESS. CLATTER OF CROCKERY AND KEYBOARD TYPING.**

**54. YOUNG MAN** George, niuzie kadi ya simu ya shilingi 500?

**55. UNCLE KILU** George, wateja wameingia, hebu nenda ukawasikilize.

**56. YOUNGMAN** George! kadi yangu iko wapi, siwezi kusubiri mwaka mzima hapa, nahitaji kupiga simu na pia kuangalia barua zangu kwenye e-mail kwa kutumia simu yangu ya mkononi.

**57. UNCLE KILU** (**SHOUTING**) George wateja….! Eeh leo…. sasa …

**58. GEORGE** Ndio, ndio mjomba (**SHOUTING TOWARDS THE CUSTOMERS**). Nitakuja sasa hivi…. kuwahudumia…!

**59. YOUNG MAN** (**TO GEORGE**) Wewe kijana mwepesi, fanya upesi!

**60. GEORGE** Hizi hapa… hizi …..!(**RUSTLE OF PACKAGING**)

**61. UNCLE KILU** Hebu niambie hizi kadi ni za kazi gani? Nawaona wateja wakizinunua kwa wingi kuzikwaruza kama kuku anayechakura mtama mchangani.

**62. GEORGE** **(CHUCKLES).** Ni kadi za muda wa maongezi kwenye simu ya mkononi mjomba. Mtu anaweza kulipia mapema muda wa maongezi kuambatana na maelewano na kampuni inayotoa huduma za mawasiliano au kununua kadi hizi….(PAUSE)…ambazo ni rahisi na nafuu kwa watu kama sisi. Sasa kwa vile tumewafungulia wateja mtandao wa intaneti kwenye simu zao za mkononi, ni vyema pia tuuze kadi hizo za simu hapa. Ni biashara nzuri!

**63. UNCLE KILU** Yaani una maana simu hizi ndogo za mkononi pia ni Komputa?

**64. GEORGE** Ndio… ndio…! Huduma hizi sio lazima uwe na komputa ndio uweze kuunganishwa. Teknolojia hii inaweza kutumika kwenye simu mbalimbali pia.

**65. UNCLE KILU** (**MUMURING AND WALKING AWAY**) Komputa….! mtandao wa intaneti na matumizi yake, kadi za simu, vyote tumejaliwa na mwenyezi Mungu,sasa kulikoni?

| | | |
|---|---|---|
| **66.** | **GEORGE** | (**BEMUSED**) Mjomba, nafikiri umekuwa ukinywa supu ya ZAPCOM. |
| **67.** | **UNCLE KILU** | Kwa hivyo…mtu yeyote mwenye simu hapa kijijini sasa anaweza kununua kadi ya simu kutoka hapa? |
| **68.** | **GEORGE** | Ndiyo sasa wanaweza kununua hapa! |
| **69.** | **UNCLE KILU** | **(SHOUTING OVER THE NOISE AND HUM**) Sikilizeni … nina habari njema kwenu nyote. (**EXAGGERATED TONE**) Kuanzia leo unapotembelea mgahawa wa Kula Tu Foods utaweza kula na kujaza muda wa maongezi kwa simu yako…. |
| **70.** | **H-SFX: LOUD LAUGHTER** | |
| **71.** | **ANNOUNCER** | AMA KWA HAKIKA MJOMBA KILU AMEKUWA MUUZAJI MASHUHURI. ANAENDELEA KUVUMBUA MBINU ZA KISASA KATIKA KUIMARISHA BIASHARA YAKE, KUPITIA TEKNOLOJIA MPYA YA MAWASILIANO KWA USHIRIKIANO WA KUNDI LA VIJANA.BIASHARA YAKE ILIYOKUWA IMEANZA KUFILISIKA SASA IMEIMARIKA TENA. |

**MUSIC: BRIDGE MUSIC**

**SCENE FOUR; UNCLE KILU'S HOME.**

**72. UNCLE KILU** Nafikiri bora tupumzike kidogo. Twendeni nyumbani kwangu tushauriane zaidi. Hapa mgahawani mtu hawezi kufikiria vizuri. Mwanangu katika siku za hivi punde unaonekana mchovu….!

**73. ZAPCOM** Ni kwa sababu ya kufanya kazi kwa saa nyingi sana...

**74. UNCLE KILU** Hali ni hiyo hiyo pia mimi, nimeanza kujisikia mchovu, upishi usiokoma karibu saa 24 kila siku…. Tunahitaji wafanyakazi zaidi iwapo biashara hii itaendeshwa usiku na mchana. Kama ujuavyo mwanangu mikono mingi hurahisisha kazi.

**75. ZAPCOM** Ni kweli Mzee.

**76. UNCLE KILU** Hebu niambie biashara hii ya huduma za mtandao wa Intaneti na simu za mkononi ni ya muda na itapita kama mitindo au ni ya kudumu?

**77. ZAPCOM** **(WITH ENTHUSIASM)** Oooh hapana Mzee. Teknolojia hii mpya ndio njia pekee ya maendeleo kote ulimwenguni. Ulimwengu sasa unakwenda kasi sana na hatuwezi kuachwa nyuma. Hii ndio njia pekee!.Subiri uone kitakachotokea baada ya kuwasili kwa teknolojia ya kutumia mkonga wa mawasiliano yaani ***Fibre Optic..***

**78. UNCLE KILU** Eti Fibre nani?

**MUSIC: THEME MUSIC**

**79. OUTRO**

**80. ANNOUNCER** Kweli elimu haina kikomo kwa mjomba Kilu. Wakati anapofikiri kwamba amejua kila kitu, mengi mazuri na mapya anayohitajika kujifunza yanaendelea kujitokeza. Amefahamu kwamba biashara yake inaimarika zaidi kwa kutumia teknolojia ya kisasa ya mawasiliano na kamwe hawezi kurudi nyuma. Je nini kitakachomtokea na washirika wake wa kibiashara? Tembelea tovuti yetu: www.dw-world.de/lbe Hadi wakati mwingine kwaheri